

## Maandamano ya Amani – Kwanini

- Wahalifu ni wao. Maandamano yasiyo ya amani yatapelekea sisi ndio tuitwe wahalifu, wachochezi, wakiuka sheria, magaidi, wavunja amani. Halafu hao tunaowapinga watahalalisha kutumia nguvu za dola dhidi yetu. Kwa hiyo maandamano yawe ya amani. Wao wabaki wahalifu na sie tubaki na haki na uhalali wetu wa kuipinga serikali dhalimu na haramu
- Maandamano yasiyo ya amani yanashirikisha watu wachache. Sio wengi wanaoweza kushiriki. Ingawaje husemwa - chachu kidogo huchachua donge zima. Inafaa wengi wetu tushiriki hizi harakati. Nguvu yetu ni wingi na umoja wetu
- Maandamano yasiyo ya amani hayawezi kudumu kwa muda mrefu. Waandamanaji watachoka - nguvu ya soda. Halafu watawala hawa dhalimu ndio wataendelea kwa kasi kubwa kututafuna. Mabadiliko ya ukweli na kudumu yanahitaji busara sio jazba sio morali. Hasira hasara
- Maandamano yasiyo ya amani yanaweza kuharibu rasimali na miundo mbinu yetu - majengo, vyombo vya usafiri, mifumo ya maji, umeme, simu n.k. vitu ambavyo tunavihitaji sisi wenyewe sasa na hapo baadae kusonga mbele. Isitoshe, kwasababu ya sera mbovu na uongozi mbaya, nchi yetu bado ni changa; tusiharibu rasilimali chache tulizonazo
- Maandamano yasiyo ya amani yanaweza kuharibu mali za watu binafsi - wafanyabiashara halali, kuleta hasara, na kuporomosha uchumi
- Utalii ni shina kubwa la uchumi wetu. Taswira za vurugu kwenye vyombo vya habari vitaharibu utalii. Washindani wetu pengine watatusikitia lakini kwa hakika watafaidika - Kenya, Rwanda, n.k. Wanaweza kutudhihaki hata kutucheka

**Jumatano, 29 Oct 2025 Siku ya Usafi wa Mazingira**

**#UsafiOyee #MazingiraOyee #SamiaMustGo**

Mjumbe Hatekwi. Mjumbe Hauwawi

- Maandamano yasiyo ya amani yanaweza kusingiziwa kuwa yanakosesha wengine nafasi / haki yao ya kupiga kura; kwamba vurugu / hofu ya ukosefu wa amani unawanyima wengine uhuru wao wa kupiga kura; kitu ambacho sio kweli hata kidogo. Waandamanaji vituo vya kura hatuvikaribii – tunaviogopa kushinda Jahannam. Kwa wale ambao kwa sababu moja ama nyingine hawataingia mtaani, **Jumatano, 29 Oct 2025 ni Siku ya Usafi wa Mazingira.** Hakuna kitu hawa mafisadi na watekaji wanaogopa zaidi kuliko vituo tupu vya kupigia kura
- Maandamano yasiyo ya amani yatafanya kuwa ngumu zaidi kazi zinazofuata baada ya kuiondoa serikali hii ya walafi, walevi wa madaraka, wabadhirifu, wachoyo, malimbukeni. Amani inahitajika kuanza kipindo cha mpito na kuhakikisha hawa miungu-mtu hawatumii ukosefu wa utulivu kupora zaidi, kuficha mali, hata kukimbia nchi
- Tanganyika imekuwa nchi ya amani toka uhuru. Si amani wanayotuhubiria viongozo uchwara ili watutawale; bali watanganyika wenyewe hulka yetu ni amani na ustaarabu. Tuendelee kubaki hivyo. Hawa malimbukeni wenye tamaa kama fisi wasituvuruge. Tusijifungulie milango ya vurugu na kuanza kuandika historia ya fujo. Angalia Zaire, Sudan, Libya, South Sudan, Somalia, Rwanda, n.k. Tusimfungulie jini kutoka kwenye chupa

- Maandamano yasiyo ya amani yana tatizo la kuweka mayai yote kwenye kapu moja. Kazi ya mabadiliko ya kweli sio ya siku moja. Hakika, ni kazi zaidi kufanya mageuzi ya amani ambayo kwa kawaida yanadai muda, umoja, jitihada, umakini

  Ni rahisi - hata kuthubutu kusema ni kuwabebesha wengine pakacha - kuandamana kwa siku chache kuliko kudumisha harakati ambazo zinatuhusu wote, zinachukua muda, kujifunga mkanda, kujitoa muhanga na sadaka

  Kadhalika, hii si kazi ya gen-z tu na wala sio ya kulibwagia jeshi. Hivyo ni busara kuandamana kwa amani kwa wingi na baada ya hapo wote kujikita katika harakati za mabadiliko

**Jumatano, 29 Oct 2025 Siku ya Usafi wa Mazingira**

**#UsafiOyee #MazingiraOyee #SamiaMustGo**

Mjumbe Hatekwi. Mjumbe Hauwawi